# Mwongozo wa Kiongozi wa Timu ya SUN - Oktoba 2023

## Kusudi

Mwongozo huu ni wa mashirika yenye wawezeshaji watakaojifunza namna ya kutoa mafunzo ya SUN. Baada ya mafunzo haya, wakati wawezeshaji watakapokuwa wakifundisha maeneo ya wenyeji kwa vikundi vidogo ya wanafunzi viziwi, kuna Mwongozo mfupi wa Mwezeshaji kwa matumizi yao.

## Kiongozi wa Timu alete vifuatavyo kwenye tukio

Seti moja ya nyenzo za kufundishia kwa kila mwezeshaji na kiongozi wa timu:

- kadi za somo 1 - 14
- ubao vidogo vyeupe, kalamu zinazofutika kirahisi ubaoni (‘marker pen’) na kifutio au kitambaa cha kufuta (kwa kutumia kipande cha karatasi au kadi zilizo kwenye karatasi za plastiki zinaweza kuchukua nafasi ya ubao mweupe)

## Ongea na Mratibu kuhusu utaratibu wa Tukio

- Idadi ya watu wanaopendekezwa kuhudhuria tukio: wawezeshaji 10 pamoja na washiriki wanafunzi viziwi (Uwiano wa kiwango cha juu cha mwezeshaji/mwanafunzi ni 1/3)

  *Wawezeshaji* ni wale wanaoweza kusoma na kutumia lugha ya alama na ambao wako tayari kuendelea kufundisha wanafunzi viziwi baada ya tukio. Wawezeshaji lazima wajitolee kuhudhuria kikamilifu siku tano za tukio.

  *Wanafunzi viziwi* ambao bado hawajajifunza lugha ya alama na kusoma, watanufaika na Mwongozo wa SUN.

- Mkalimani wa lugha ya alama kwa ajili ya lugha inayozungumzwa na wenyeji atahitajika
- Usafiri, chakula, na malazi kwa viongozi wa timu, wakalimani, wawezeshaji, wanafunzi
- Ubao mkubwa mweupe (‘marker pen’/kifutio au kitambaa) au ubao wa chaki (chaki/kifutio)
- Pedi ya karatasi zenye ukubwa wa chati/kalamu ya wino mzito
- Bunda la karatasi za nakala
- Vibandiko vya majina, pedi za karatasi au daftari, na penseli au kalamu ya wino kwa wote waliohudhuria
- Kadi za faharasa, kadi za karatasi ngumu, au karatasi kutengeneza kadi za alama za masomo mapya
- Ikiwezekana: penseli za rangi za kadi za alama kwa masomo mapya
- Jozi 3 au 4 za mkasi
- Chapisha: Kitabu cha SUN cha Marko, Kamusi ya Msomaji wa SUN, na Kitabu cha Somo cha Mwezeshaji wa SUN kwa wawezeshaji wote. **Tafadhali subiri kusambaza. Mwongozo wa kufundisha utaelekeza wakati wa kufanya hivi.** Tafuta toleo la karibuni katika www.sun.bible
- Chapisha: vyeti vitakavyojazwa na Mratibu wa Tukio na kutiwa saini na Kiongozi wa Timu ya SUN

## Ratiba ya tukio

**Ili kufundisha kwa kutumia nyenzo zote vizuri kwa siku tano, ni muhimu kupanga saa nane za kazi kila siku (muda huu hauhusishi ule wa chakula mchana na mapumziko).**

Timu ya wenyeji itakuwa na jukumu la kupanga ibada za asubuhi kwa kila siku. Inapendekezwa kuwa timu mwenyeji iteue mtunza muda kwa ajili ya kuanza kwa wakati asubuhi na baada ya mapumziko/chakula cha mchana, kuzuia majadiliano marefu, nk.

Ratiba ifuatayo ya kila siku imeandikwa kwa ajili ya wawezeshaji na wanafunzi kuwasili Siku ya 1.

Kipindi cha 1 na 2 cha kila siku ni mwongozo wa asubuhi kwa wawezeshaji (wanafunzi wanaweza angalia tu wakati wa tukio hilo au kuwa na shughuli mbadala). Wafanye wawezeshaji wakae pamoja karibu na kiongozi wa timu wakati wa mafunzo.

Kipindi cha 3 na 4 cha kila siku ni cha mchana na kimsingi ni cha kuwaandaa wawezeshaji kuwa na uzoefu wa kufundisha kwa vitendo na mazoezi kwa wanafunzi, wanaoingia vipindi hivyo.

Kila kipindi hupaswa kuchukua kama saa 2. Inapendekezwa mapumziko mafupi au chakula cha mchana kati ya vipindi hivyo . Shughuli nyingi kuu zinapaswa kuchukua dakika 30 kila mmoja-kama vile tukio la ufunguzi wa kila siku, kufundisha somo, na kuhakiki michezo.

Mratibu mwenyeji anaweza kupendekeza ratiba ambayo wawezeshaji wawasili siku ya 1 na wanafunzi hufika Siku ya 3. Hilo likitokea, marekebisho ya mpango wa mafunzo huhitajika, lakini yakihakikisha kwamba vipindi vyote vya kufundisha vinavyohusisha wawezeshaji na vile kati ya wawezeshaji na wanafunzi vinajumuishwa katika ratiba.

# SIKU YA 1

**Katika mwongozo huu, maneno yaliyo katka mwandiko wa *italiki* ndiyo utakayosema kwa wawezeshaji.**

Malengo ya siku: Jifunze alama za msingi. Utangulizi kuhusu SUN, fundisha somo la 1 - 5 na kadi za sentensi zinazolingana, jifunze kuandika alama, mchezo wa mapitio ya alama (kuandika alama kwenye viganja), wawezeshaji kufanya mazoezi ya kuwafundisha wanafunzi masomo ya 1 - 4 na kufanya mchezo wa mapitio ya alama nao, tambulisha Mpango wa Timu.

## KIPINDI CHA 1

Ufunguzi – wimbo wa ibada, ibada fupi, sala na makaribisho yakiongozwa na timu mwenyeji. Utambulisho wa viongozi wa timu, wakalimani, wawezeshaji, wanafunzi. Taarifa zinaweza kutolewa kama vile miongozo ya mitandao ya kijamii iwapo kuna sababu za kiusalama, ratiba ya kila siku, upatikanaji wa maji, vyoo, nk.

Utangulizi kuhusu SUN
*Symbolic Universal Notation (SUN) ni mfumo wa ya picha, michoro au alama kwa ajili ya Viziwi ambao hawakupata fursa ya kujifunza kusoma au kuandika. Mfumo huu unaweza kutumika duniani kote kutokana na sifa ulizo nazo:*

***Rahisi na haraka kujifunza*** *- Mfumo huu unaweza kujifunza haraka kiasi cha kuwezesha kuanza kusoma Maandiko baada ya masomo machache ya utangulizi. Haulazimishi kutumia miaka mingi kukuza uwezo wa kusoma na kuandika kabla ya kuweza kuyafikia Maandiko.*

**Kufahamika** - *Kadiri ya alama zinavyofahamika zaidi, ndivyo zinavyokuwa rahisi kujifunza na kuzikumbuka.*

***Zinafahamika duniani*** - *Baadhi ya alama, ambazo hazifahamiki katika maeneo mengine ya dunia, huhitaji kukariri. Hizi zipo chache kadiri iwezekanavyo ili kutolazimisha seti mpya ya alama kwa kila lugha na tamaduni.*

*SUN ina seti kuu ya alama za msingi. Alama hizi hugeuzwa au huunganishwa kutengeneza alama nyingine (maneno mapya)*

Andika kwenye ubao mweupe au karatasi ya chati:

Alama ya Msingi, Badilifu, Mchanganyiko

Chini ya **Alama ya msingi** *chora* alama ya "mtu" 

- *Hii inaweza isionekane kama mtu, lakini ikiwa unafikiria kuongeza uso wa tabasamu na mikono, itafanana na mtu.*

Chora alama ya "kalamu" 

- *Hii inaweza isionekane kama "kalamu/penseli, lakini iwapo utaongeza ncha na kifutio, itaonekana kama penseli*.


Chini ya mchoro **Badilifu** chora alama ya "mtu" lakini igeuze ili alama iwe "kulala" 

- *Kwa kugeuza au kubadilisha alama ya msingi ya "mtu", inakuwa alama ya "kulala"*.

Chora alama ya "mtu" na kuongeza "mikono iliyonyooshwa" 大

- *Kufanya mabadiliko hayo madogo kwa "mtu" inakuwa alama ya "kubwa."*

Chini ya **Mchanganyiko** chora alama ya "mtu" na "kalamu" ziweka pamoja, bila kuacha nafasi kati yao.

人 

- *Kuchanganya alama "mtu" na "kalamu" hufanya hutengeneza neno "mwandishi au mtunzi."*

Chora alama ya Mungu 

- *Wakati mshale mdogo unapoongezwa upande wa juu kushoto wa alama mchanganyiko, hii inaonyesha nomino, jina mahususi la mtu, mahali, au kitu. Alama hii ni mchanganyiko wa mwanadamu, upendo, baba na mfalme. Unafikiri utaleta jina gani?*

*Hivi ndivyo mfumo wa SUN unavyoundwa. Unategemea alama 100 za msingi ambazo badilifu au mchanganyiko na kutengeneza alama nyingine zote. Kwa njia hii, inafanya iwezekane kuwakilisha maneno yote ya Agano la Kale na Maneno ya Agano Jipya yenye lugha ya SUN!*

*Tutashughulikia alama zote za msingi wakati wa vipindi vya asubuhi siku mbili za kwanza, na siku tatu za mwisho tutafanyia kazi kwa karibu zaidi na alama badilifu na mchanganyiko na umuhimu wa kuandaa mipango ya somo la Maandiko. Katika vipindi vya mchana, utafanya mazoezi kufundisha vikundi vidogo vya wanafunzi.*

<u>Jinsi ya Kufundisha kwa kutumia Kadi za Somo (Somo la 1)</u>
*Kujifunza alama za msingi kunaweza kulinganishwa na kujifunza alfabeti kabla ya kujifunza somo*. *Vivyo hivyo, alama za msingi* <u>*zinahitaji kujifunza vizuri*</u> *kwasababu hutumika kutunga maneno yote ya Biblia!*

Hatua ya 1. Waonyeshe wawezeshaji kadi ya somo la kwanza lenye alama. Waambie wafikirie sekunde chache kuhusu maana, inaweza kuwa (hakuna haja ya kujibu, wafikirie tu maana).

Hatua ya 2. Onyesha mara moja upande wa picha wa kadi ili kuepusha wawezeshaji kukosea kile wanachohusisha na alama akilini mwao. Onyesha na jizoeze lugha ya alama itakayotumika kwa wenyeji. Ikiwa zipo maana nyingi za alama, fundisha maana, na lugha ya alama.

Hatua ya 3. Rudia hatua ya 1 na 2 kwa kadi 4 zinazofuata.

Hatua ya 4. Baada ya kadi 5 kufundishwa, changanya kadi na uhakiki ukitumia upande wa alama kadi pekee. Wawezeshaji wanapaswa kujibu alama sahihi. Tumia upande wa picha ikiwa tu wawezeshaji hawakumbuki maana ya alama.

Hatua ya 5. Rudia hatua ya 1 na 2 kwa kadi 5 zilizosalia katika somo.

Hatua ya 6. Pitia kadi hizi (6 - 10) kwa njia sawa na hatua ya 4.

Hatua ya 7. Onyesha kadi ya sentensi ya kwanza. Waambie wawezeshaji kuitaja (lugha ya alama) sentensi wakati ukielekeza kila alama.

Hatua ya 8. Waambie wachague picha sahihi inayoonyeshlugha ya aolla sentensi. Hii ni tathimini ya ufahamu.

Hatua ya 9. Rudia hatua ya 7 na 8 kwa sentensi nyingine za somo.

Hatua ya 10. Changanya kadi zote na upitie alama na lugha ya alama zote za somo la kwanza.

Waambie wawezeshaji wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe. Angalia usahihi itakapohitajika—alama zinahitaji kuandikwa sawa na kwenye kadi. Hili ni muhimu kwani watakuwa wakiandika sentensi na fanya kadi za alama mchanganyiko kwani Maandiko mapya baadaye katika mafunzo hayo! (tumia si zaidi ya dakika 5 kwa hili)

Fundisha Somo la 2 kwa kutumia hatua 1 - 10, kwa Hatua ya 10 pitia kadi zote ulizojifunza katika masomo mawili ya kwanza. Mapitio ni muhimu ili kusaidia kukumbuka maelezo. Wawezeshaji wajizoeze kuandika alama, angalia usahihi.

## KIPINDI CHA 2

Fundisha Somo la 3 kwa kutumia hatua 10 za kufundishia, kwa Hatua ya 10, pitia kadi za Masomo 1-3. Wawezeshaji wafanye mazoezi ya kuandika alama, angalia usahihi.

Mchezo wa mapitio: Chora alama kwenye viganja
Tengeneza timu za watu 5 kila moja. Timu zinasimama kwenye mstari, zote zikitazama mbele. Mpe mtu wa kwanza katika mstari ubao mweupe au karatasi na kalamu ya wino mzito.

- Kiongozi wa timu anamuonyesha mtu wa mwisho kwenye mstari kadi ya alama kutoka kwenye masomo yaliyofundishwa asubuhi hii. Ni bora kuanza na alama rahisi kwanza. Hakikisha hakuna mtu mwingine kwenye timu aliyeiona!
- Kwa kidole chake, mtu huyo huchora alama kwenye kiganja cha mtu aliye mbele yake mstalini. Wanaweza kurudia mara moja ikiwa inahitajika, kisha wageuke kuelekea upande mwingine.
- Mtu aliyepokea mchoro kisha huchora kile alichoelewa kwa alama kwenye kiganja cha mtu aliye mbele yao na anaweza kurudia mara moja ikihitajika na kisha geuka kuelekea upande mwingine.
- Mchezo unaendelea hivi hadi mtu wa mwisho awe amepokea mchoro wa kiganja, kisha huchora alama aliyoelewa kwenye ubao mdogo mweupe au kipande cha karatasi.
- Kiongozi wa timu kisha huwaambia wageuke. Mtu kwa kila timu iliyochora alama kwenye ubao wao mweupe au karatasi huonyesha mchoro wao.
- Kiongozi wa timu anaonyesha kadi ya alama na kutoa pointi moja kwa kila timu ikiwa alama yao ilichorwa kwa usahihi.
- Mtu aliyechora kwenye ubao mweupe au karatasi huenda hadi mwisho wa mstari. Rudia mchezo hadi kila mtu awe na zamu ya kuchora alama ya mwisho kwa timu yao.Endelea kutoa pointi.
- Njia mbadala ya kucheza: mtu anayepokea mchoro kwenye kiganja chake afumbe macho!

Fundisha Somo la 4 kwa kutumia hatua 10 za kufundishia, kwa Hatua ya 10 pitia Somo la 2 - 4 (Masomo 3 ya mwisho). Wawezeshaji hufanya mazoezi ya kuandika alama, angalia usahihi.

Fundisha Somo la 5 kwa kutumia hatua za kufundishia, kwa kadi za mapitio za Hatua ya 10 Somo la 3 – 5 (Masomo 3 ya mwisho). Wawezeshaji hufanya mazoezi ya kuandika alama, angalia usahihi.

## KIPINDI CHA 3

Gawa Kitabu cha Somo cha Mwezeshaji wa SUN na kadi za somo 1 – 14 kwa kila mwezeshaji

*Mchana wa leo utaanza kufundisha vikundi vidogo vya wanafunzi Masomo ya 1 - 4 ambayo wewe ulijifunza asubuhi ya leo. Kasi ya ufundishaji iendane na mwitikio wa wanafunzi kuelewa somo. Kwa madhumuni ya kufundisha katika tukio hili, utafundisha masomo kwa hatua za haraka zaidi kuliko ungefanya unapofundisha wanafunzi mahali waliko.*

- *Wanafunzi wanatakiwa kutumia lugha ya alama kwa alama wanazofundishwa ili hakikisha waelewe.*
- *Wakati lugha ya alamo (kikanda) zinapotumika wakati wa semina wanafunzi wataweza kuwasiliana vyema na viziwi wengine.*
- *Kuwa mwangalifu harakati zako za mikono zisizo lazima zisiwachanganye wanafunzi.*

Mpe kila mwezeshaji kikundi kidogo cha kufundisha, ikiwezekana wanafunzi 2 au 3. Ruhusu muda zaidi kuhimiza vikundi vipya vichangamane, kujifunza alama za majina, n.k.

Wawezeshaji fundisha Somo la 1 na la 2 kwa kufuata hatua za ufundishaji walizojifunza katika vipindi vya asubuhi. Wanafunzi waambie wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe. **Ni muhimu kwamba viongozi wa timu waangalie, wasaidie, watoe maoni, wahimize, wajibu maswali, n.k. wakati huo.**

Mchezo wa Mapitio: Chora alama kwenye viganja vya mikono - unganisha vikundi vidogo katika timu (sio zaidi ya 4 au 6 kwenye timu) kucheza mchezo ambao wawezeshaji walijifunza asubuhi. Wawezeshaji wanaongoza shughuli na wanaweza kwanza kuonyesha jinsi mchezo unavyochezwa.

## KIPINDI CHA 4

Wawezeshaji fundisha Somo la 3, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Somo la 1 -3. Wanafunzi waambie wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe.

Wawezeshaji fundisha Somo la 4, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Masomo 2-4 (masomo 3 ya mwisho). Wanafunzi waambie wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe.

Mrejesho na Maswali/Muda wa majibu na wawezeshaji

Mipango ya Timu
Nyuma ya Mwongozo wa Kiongozi wa Timu kuna kitini cha Mpango wa Timu ili kuwaongoza wawezeshaji kuandaa mipango na malengo ya baada ya semina kwa ajili ya timu yao. Hii itakuwa kazi ya nyumbani au, iwapo muda unaruhusu, inaweza kufanywa mwishoni mwa siku ya kazi ikiwa kuna muda wa ziada uliobaki. Wao watashiriki mipango yao siku ya mwisho na kuwasilisha mpango ulioandikwa kwa kiongozi wa timu.

Eleza jukumu la Timu ya Uongozi ambayo imeorodheshwa kwenye Mpango wa Timu kwenye kitini.

Himiza ushiriki wa jamii na kanisa kusaidia SUN eneo walipo na kwa njia endelevu.

Kufunga - Amua nani ataongoza ibada ya kesho ya ufunguzi, ibada fupi, na maombi. Hitimisha siku kwa wimbo wa kuabudu wa furaha na maombi.

# SIKU YA 2

Malengo ya siku: Maliza kujifunza alama za msingi. Fundisha masomo ya 6 – 10 na kadi sentensi zinazolingana, fanya mazoezi ya kuandika alama, jadili njia tofauti za kufundisha alama ambazo zina maana ngumu zaidi, mchezo wa mapitio ya alama mpya (picha), wawezeshaji wajizoeze kufundisha somo la 5 – 8 na wanafunzi na ufanye nao mchezo wa leo wa mapitio.

## KIPINDI CHA 1

Ufunguzi – wimbo wa ibada, ibada fupi, sala inayoongozwa na timu mwenyeji; matangazo kama yapo

*Asubuhi ya leo tutafanya masomo mengine matano zaidi kisha utakuwa umejifunza alama zote za msingi pamoja na namba! Tutajadili* njia tofauti za kufundisha alama ambazo zina maana ngumu zaidi, *na ujifunze mchezo mpya wa mapitio.*

Fundisha Somo la 6, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Somo la 4 - 6 (masomo 3 ya mwisho). Wawezeshaji wafanye mazoezi ya kuandika alama, angalia usahihi.

Fundisha Somo la 7, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Somo la 5 - 7 (masomo 3 ya mwisho). Wawezeshaji wafanye mazoezi ya kuandika alama, angalia usahihi.

Mapitio ya mchezo: Picha
Wagawe wawezeshaji katika timu mbili. Ipe kila timu ubao vidogo vyeupe au karatasi na kalamu ya wino mzito.
*Wakati wa kujifunza lugha, kama vile SUN, kuandika daima ni ngumu zaidi kuliko kusoma. Ikiwa unaweza kuandika neno, utakuwa umeelewa kweli. Kwa hivyo, tutapitia leo kwa kuandika alama kutoka kumbukumbu zetu.*

- *Msaidizi atataja kwa lugha ya alama mojawapo ya alama kutoka kwa masomo ambayo tumejifunza hadi sasa. Mwandishi wa timu yako ataandika alama kutoka kwenye kumbukumbu na kuinua mkono akimaliza.*
- *Waandishi wote wawili watakapomaliza, mtu aliyeinua mkono kwanza ataangaliwa kwanza. Ikiwa alama imeandikwa kwa usahihi timu yao inapata pointi tatu.*
- *Ikiwa alama imeandikwa vibaya, timu nyingine inaangaliwa na kama alama imeandikwa kwa usahihi timu yao inapata pointi mbili.*
- *Ikiwa hakuna timu itakayopatia, msimamizi ataonyesha jibu, na kutoa pointi moja kwa timu kwa jaribio bora.*
- *Kila mtu atakuwa na zamu ya kuwa mwandishi. Chagua nani atakuwa wa kwanza kwa timu yako.*

## KIPINDI CHA 2

Fundisha Somo la 8, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Somo la 6 - 8 (masomo 3 ya mwisho). Wawezeshaji wafanye mazoezi ya kuandika alama, angalia usahihi.


Majadiliano
*Somo la 6, 7, na 8 limetoa dhana ngumu zaidi.*
- *Je, ni dhana gani kutoka masomo haya matatu, ambazo unadhani ni ngumu zaidi?* (laini,tamu, kazini, kushoto, n.k. Orodhesha alama ambazo wawezeshaji wanapendekeza kwenye ubao mweupe/karatasi ya chati.)


- *Je, ni mawazo gani unaweza kufikiria kuongeza kama mafundisho ya ziada kuhusu dhana hizi iwapo unadhani picha iliyo nyuma ya kadi ya alama haitoshi kwa wanafunzi wako kuelewa maana kikamilifu?*
- *Kumbuka kwamba lugha ya alama ni mpya kwa wanafunzi wengi. Kwa hiyo ungewezaje kuwasaidia kupata ufahamu mzuri wa dhana husika?*
- Katika vikundi vidogo, waambie wawezeshaji wajadiliane na kuja na suluhu zao wenyewe kwa Dakika chache, kisha waambie wabadilishane mawazo na kundi zima. (Baadhi ya mawazo ni kuigiza, kuchora picha, kutumia 'props'/ vitu, tumia utafutaji wa google kwenye simu zao,na kadhalika.)


Ruka Somo la 9 na fundisha Somo la 10 – Alama ya watu inaongoza jinsi ya kuandika wingi. Alama ya mwanamke si alama ya msingi bali ni alama badilifu kutoka mwanaume. Kwa Hatua ya 10, pitia kadi za Somo la 7, 8, na 10. Wawezeshaji wajizoeze kuandika alama, angalia usahihi. Hakuna kadi za sentensi kwa somo hili.


Fundisha Somo la 9 – kwa Hatua ya 10, pitia kadi za somo 8, 9, na 10.
Baada ya kufundisha somo la 9, endelea kufundisha namba zilizoizidi kumi.


*Hapa kuna mifano michache ya jinsi namba kubwa zaidi kuliko 10 zinavyoandikwa katika* SUN.
Andika namba zifuatazo kwenye ubao mweupe au karatasi ya chati:

Andika alama za 12  *Hii ni SUN kwa namba 12*.

Andika alama za 23  *Hii ni SUN kwa namba 23.*

Andika alama za 145  *Hii itakuwa namba gani?*

Andika alama za 600  *Hii itakuwa namba gani?*

Andika alama za 9013  *Hii ni SUN kwa nambari 9013.*

Pitia kadi zote Masomo 1 – 10 ikiwa muda unaruhusu. Uhakiki huu unapaswa kwenda haraka na kuchukua tu dakika chache maana wawezeshaji wanapaswa kuzijua vizuri kufikia sasa.

## KIPINDI CHA 3

Wawezeshaji Kufundisha kikundi kile kile kidogo cha wanafunzi ambacho walikuwa nao jana. Ni muhimu kwamba viongozi wa timu wanaendelea kuwepo kuangalia, kusaidia, kutoa maoni, kuhimiza, kujibu maswali, nk wakati huo. Hata hivyo, wakati wawezeshaji wanazidi kupata uzoefu wa kufundisha, wewe unapaswa kutoa kiwango cha juu cha uhuru na hitaji dogo la usaidizi/kufundisha.

Wawezeshaji kufundisha Somo la 5, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Somo la 3 – 5. Wanafunzi waambie wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe.

Wawezeshaji kufundisha Somo la 6, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Somo la 4 – 6. Wanafunzi waambie wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe.

Fanya mapitio ya haraka ya Somo la 1 na 2 kabla ya kucheza Mchezo wa Picha.

Mchezo wa mapitio: Picha – Kwa kutumia kadi za alama kwa Somo la 1 – 6, unganisha vikundi vidogo katika timu (si ya zaidi ya watu 5 au 6 kwenye timu) kucheza mchezo ambao wawezeshaji walijifunza katika kipindi cha asubuhi. Unaweza kurahisisha jinsi ya kutoa pointi. Wawezeshaji wataongoza shughuli na wanaweza kufanya onyesho la jinsi mchezo unavyochezwa.

## KIPINDI CHA 4

Wawezeshaji kufundisha somo la 7, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Somo la 5 – 7. Wanafunzi waambie wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe.

Wawezeshaji kufundisha Somo la 8, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 Somo la 6 – 8. Wanafunzi waambie wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe.

Shughuli ya mapitio – Fanya kundi moja kubwa la wawezeshaji na wanafunzi au ugawanye katika vikundi viwili ikiwa kuna nafasi ukumbini. Onyesha kadi ya alama na lugha ya alama na kisha kuigiza hilo neno.

Mrejesho na Maswali/Muda wa ajibu na wawezeshaji

Mipango ya Timu – Uliza kama wamepata muda wa kuanza majadiliano na timu yao.Je, wana maswali yoyote? Wakumbushe wao watashiriki mipango yao siku ya mwisho na kuwasilisha mpango ulioandikawa kwa kiongozi wa timu. Ikiwa muda unaruhusu kabla ya kufunga, wape muda wa kulifanyia kazi hilo.

Kufunga – Amua nani ataongoza ibada ya kesho ya ufunguzi, ibada fupi, na maombi. Hitimisha siku kwa wimbo wa kuabudu wa furaha na maombi.

# SIKU YA 3

Malengo ya siku: Misingi ya sarufi ya SUN, wawezeshaji kuandika sentensi fupi, michezo ya mapitio(namba), fundisha somo la 11 na 12 ambalo hutambulisha alama mchanganyiko, Kamusi ya Msomaji wa SUN, mapitio ya mchezo/shughuli (Kushindana), wawezeshaji wafanye mazoezi ya kufundisha somo la 9 -12 na wanafunzi na fanya mapitio ya mchezo wa namba.

## KIPINDI CHA 1

Ufunguzi – wimbo wa ibada, ibada fupi, sala inayoongozwa na timu mwenyeji; matangazo kama yapo

Kuandika Sentensi katika SUN

***Kama ilivyo kwa lugha zote kuwa na muundo wake wa kipekee, ndivyo ilivyo kwa SUN.***

*Muundo wa sentensi wa jumla: Katika kusoma SUN, muktadha, au wazo kuu, ndicho kitu muhimu kwa ufahamu. Kazi ya mwezeshaji ni kufundisha wanafunzi jinsi ya kusoma maandishi ya SUN ili waweze kuelewa maana vizuri zaidi. Mwezeshaji hapaswi kufundisha muundo wa sarufi unaopatikana katika lugha yao bali kufundisha muundo wa sarufi ya SUN kwa sababu Biblia ya SUN imeandikwa kwa kutumia sarufi hii. Hata kama mpangilio wa maneno katika sentensi za SUN haujulikani, bado utakuwa unaeleweka.*

*Asubuhi ya leo utafanya mazoezi ya kuandika sentensi katika SUN. Kwa kutumia alama ambazo wewe umejifunza katika somo la 1 - 10, utaandika sentensi 3 zenye angalau alama 3 katika kila moja ya sentensi. Kabla ya kuanza, hebu tuzungumze kidogo kuhusu sarufi ya SUN.*

***Mpangilio wa alama katika sentensi:*** *Kama kanuni ya jumla, sentensi hufuata mpangilio huu: Mtenda, Kitenzi, Mtendwa/Kitendwa [direct object] (kama sentensi ni amri, inaweza kuanza na kitenzi, kama vile "weka matunda mezani")*

*Vivumishi kabla ya nomino, vielezi kabla ya kitenzi*

***Urefu wa sentensi****: Urefu wa sentensi si zaidi ya alama 7*

***Wingi:*** *Alama huandikwa mara mbili bila nafasi kati yao* (andika mifano kwenye ubao mweupe - watu kama katika somo la 10……, upanga …..)

***Umilikishi****: Inaonyeshwa kwa nukta kubwa nyeusi kwenye sehemu ya juu ya kulia ya alama. Weka kimilikishi kabla ya kitu wanachomiliki au walicho nacho.* (andika mfano kwenye ubao mweupe kwa "pua ya nguruwe")



Mpe kila mwezeshaji nusu karatasi ya chati au kipande cha karatasi na 'marking pen' au matumizi mbao ndogo nyeupe.

*Unapaswa kuandika sentensi 3 za SUN zenye angalau alama 3, ukitumia* alama *za somo la 1 – 10 lakini zisizidi alama 7 katika kila sentensi. Tumia kanuni za msingi za sarufi ya SUN. Tafadhali andika kwa ukubwa wa kutosha ili kurahisisha ushirikishaji wa sentensi kwa kikundi kidogo. Utakuwa na dakika 10 - 15 kukamilisha sentensi zako 3. Je, una maswali yoyote kabla ya kuanza?*

Baada ya dakika 10 - 15 (hata kama hujakamilisha sentensi zote 3), gawanya katika makundi mawili madogo yenye kiongozi wa timu kwa kila kundi.

- Kila mwezeshaji ataonyesha sentensi yake.
- Mwezeshaji mwingine atasoma na kueleza sentensi kwa lugha ya alama.
- Ikiwa maana haieleweki, muulize mwezeshaji kile walichokusudia kusema na kuwasaidia kuchagua alama sahihi.
- Kiongozi wa timu anapaswa kutoa maneno ya faraja na mapendekezo kadiri inavyofaa.

Mapitio ya mchezo: Namba

1. Weka kadi za alama za namba kwenye sakafu au ukuta, tawanya kuzunguka eneo kubwa.
2. Taja namba (lugha ya alama) 0 -10 na wawezeshaji kukimbia/kutafuta kuona ni nani anayeweza kupata kadi za alama inayolingana kwenye sakafu au ukuta kwanza.
3. Endelea na namba zingine.
4. Mabadiliko: kwa hatua ya pili, mpe kila mwezeshaji nambari 0 -10 kadi na waambie wote wakatafute kadi zenye alama za namba walizo nazo kwenye sakafu au ukuta.
5. Shughuli ya ziada: mpe kila mwezeshaji kadi ya alama ya namba na wanatengeneza mstari kwa mpangilio 0 - 10. Changanya kadi, rudia zoezi.

## KIPINDI CHA 2


*Jana ulijifunza alama za msingi zilizobaki. Kuna masomo mawili zaidi yenye alama mpya, lakini zitakuwa alama badilifu na mchanganyiko si alama za msingi. Asubuhi ya kwanza, alama badilifu na mchanganyiko zilitambulishwa. Je, kuna mtu angependa kutuambia kuhusu alama badilifu na mchanganyiko?* (Iwapo wamesahau, fanya mapitio ya haraka.)

Fundisha Somo la 11, kwa kadi za mapitio ya Hatua ya 10 kwa Somo la 9 - 11.

Fundisha Somo la 12 – Unapofundisha alama za Mungu na Yesu, wakumbushe kwamba mshale mdogo juu unamaanisha alama ni nomino sahihi. Kwa hatua 10 fanya mapitio ya kadi somo la 10 - 12.




Mchezo wa mapitio: Kutambua alama badilifu na mchanganyiko zilizoainishwa na alama za msingi
Wagawe wawezeshaji katika timu mbili au tatu.


- *Nitakuonyesha alama ya msingi na timu yako itaandika alama badilifu au mchanganyiko kutoka somo la 11 na 12 ambalo lina alama za msingi.*
- *Kwa mfano, alama ya msingi ya mlango iko katika alama hizo badilifu na mchanganyiko:*






 Andika haya kwenye ubao mweupe.


- *Timu hupata pointi kwa kila alama sahihi badilifu au mchanganyiko wanayoandika kwa dakika moja.*

Alama za msingi za kutumia na alama badilifu na au mchanganyiko kwa kila moja:

hapana  - (kufungua)  (bubu)  (kiziwi)  (huru) 

upendo  - (tamani)  (kuombaomba)  (Mungu)  (mbinguni) 

mdomo  - (bubu)  (ulimi)  (kutema)  (alipumua)  (kuombaomba) 

kitu  - (mbali)  (juu ya)  (katika)  (kuweka)  (kugusa)  (kuleta)  (ulimi) 

Kamusi ya SUN

**Onyesha kamusi yako, ila kumbuka muda wa kutoa kamusi za wawezeshaji vado haujafika.**

*Hii ni Kamusi ya SUN ya alama zote katika Agano la Kale na Jipya isipokuwa kwa baadhi ya majina ya Agano la Kale. Utatumia hii kuandaa masomo mapya ya Maandiko kwa wanafunzi wako. Kamusi imepangwa kwa alama za msingi ambazo zimefundishwa (pamoja na zingine chache). Zifuatazo ni sehemu kuu za kamusi.*

Onyesha kila sehemu kwa ufupi.

- ***Jedwali la Yaliyomo*** *lina alama zote za msingi na huonesha namba za kurasa za kutafuta alama badilifu na mchanganyiko ambazo zina jumuishi alama hizo za msingi.*
- ***Alama za msingi zilizo na chati ya alama zake zilizo badilifu na mchanganyiko*** *ndizo zinazofuata. Alama ya mtu ni ya kwanza na ina kurasa 5. Chati za alama zingine zinaweza kuwa fupi na sehemu tu ya ukurasa, kama vile alama “mimi” ambayo hufuata kurasa za mtu.*
- *Kurasa za* ***Mishale, namba, na vituo*** *hufuata alama zote za msingi.*
- ***Kurasa za Nomino Sahihi*** *zipo mwishoni mwa kamusi na zimepangwa katika kategoria 7: Mungu, mwanaume, mwanamke, ardhi/mlima/bonde/kisiwa, kijiji, mto/maji, nyinginezo. Kumbuka alama hizi zote zina mshale mdogo upande wa juu kushoto alama zao kukuwezesha ujue kuzitafuta katika kurasa maalum za Nomino Sahili.*
- **Kielezo** - sehemu ya maneno ya kawaida na sehemu ya nomino sahihi

Mpe kila mwezeshaji Kamusi ya SUN.

*Baada ya kuangalia kamusi yako kwa dakika chache tutafanya mazoezi pamoja ya jinsi ya kuitumia.*

*Ukurasa wa kwanza ni "Jinsi ya kuitumia Kamusi ya Msomaji ya SUN." Tutaipitia pamoja na kujizoezesha kwa mifano iliyotolewa katika kamusi hiyo.*

Andika alama chache rahisi kwenye ubao mweupe au karatasi kama vile mchungaji ….. , zaka ….., na baadhi ya majina kutoka sehemu za Nomino Sahili ili wazitafute katika Kamusi. Kwa sababu orodha ya majina yanayotokana na mwanaume ni ndefu, kuanza na jina la mwanamke ni rahisi zaidi! Wakumbushe kwamba ikiwa kuna mshale mdogo upande wa juu kushoto wa alama mchanganyiko watakuwa wanatafuta katika sehemu za Nomino Sahihi.

Shughuli/mchezo: Kushindana

Chagua alama mchanganyiko kutoka kamusi na uiandike kwenye karatasi au ubao mweupe. Shindanisha na tazama ni nani anayeweza kuwa wa kwanza kuipata. Uliza ni ukurasa gani wa ishara walipata mchanganyiko. Fanya mazoezi machache tena kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kutumia kamusi.

## KIPINDI CHA 3

Wawezeshaji wanaendelea kufundisha kundi lile lile dogo la wanafunzi.

Kuandika Sentensi katika SUN - Tumia alama ambazo wamejifunza katika somo la 1 - 8 (au tu kupitia somo la 6 ili kurahisisha kazi kidogo). Onyesha mifano miwili au mitatu kwao.

Fundisha Somo la 10 - kwa Hatua 10, fanya mapitio ya Somo la 8 - 10. Wanafunzi waambie wajizoeze kuandika alama kwenye karatasi au ubao mweupe.

Fundisha Somo la 9 - Baadhi ya wanafunzi wanaweza wasiwe na uzoefu mkubwa wa dhana za namba. Iwapo ni hivyo, fundisha somo hili kama "kumbukumbu ya kukariri." Dhana za namba zinaweza kuchukua muda kuzielewa. Kwa Hatua 10, fanya mapitio ya Somo la 7 - 9.

Mapitio ya mchezo: Namba

**KIPINDI CHA 4**

Fundisha Somo la 11 – kwa Hatua 10, fanya mapitio ya Somo la 9 - 11.

Fundisha Somo la 12 – Kwa alama ya Mungu na Yesu, huu ni wakati mzuri wa kuwafundisha wanafunzi kishale cha juu upande wa kushoto kinatumika kuonyesha jina. Kwa Hatua 10, fanya mapitio ya Somo la 10 - 12.

Mrejesho na Maswali/Muda wa Majibu na wawezeshaji

Mipango ya Timu – Uliza kama wamepata muda wa kuanza majadiliano na timu yao.Je, wana maswali yoyote? Wakumbushe wao watashiriki mipango yao siku ya mwisho na kuwasilisha mpango ulioandikawa kwa kiongozi wa timu. Ikiwa muda unaruhusu kabla ya kufunga, wape muda wa kulifanyia kazi hilo.

Kufunga - Amua ni nani atakayeongoza ibada ya kesho ya ufunguzi, ibada fupi, na maombi. Maliza siku kwa wimbo wa kuabudu wa furaha na maombi.
The sixth bullet on this page is for “large white board”...in this bullet, it needs to say “small white board”

# SIKU YA 4

Malengo ya siku: Fundisha somo la 13 (uwekaji alama za vituo na hadithi ya kwanza ya Maandiko), fundisha alama mpya mchanganyiko, shughuli/mchezo (alama mpya mchanganyiko), kuandaa kufundisha Maandiko mapya, fundisha somo la Wokovu, wawezeshaji wajizoeze kufundisha somo la 13 kwa wanafunzi na kuigiza.

## KIPINDI CHA 1

Ufunguzi – wimbo wa ibada, ibada fupi, sala inayoongozwa na timu mwenyeji; matangazo kama yapo.


Fundisha Somo la 13
*Sasa tuko tayari kusoma Maandiko kwa SUN!*


*Alama za vituo hutumika katika hadithi. SUN ni lugha ya maandishi, na tunafundisha kusoma na kuandika.Wanafunzi ambao hawajapata uzoefu wa kusoma wanahitaji kuzielewa alama za vituo.*


*Kadi za kufundishia kwa Somo la 13 zina kadi 8: nukta, koma, nukta ya mshangao, alama ya kuuliza, alama za kunukuu, alama za nukuu moja, kimilikishi, na kiashiria cha jina sahihi. (Haya ni marejeo mazuri kwa wawezeshaji lakini si ya kutumiwa na wanafunzi.)*


*Kwa wanafunzi, wakifundishwa alama za vituo katika muktadha kutakuwa na maana zaidi. Kabla kusoma hadithi ya Maandiko pamoja nao, alama hizi za vituo zinapaswa kufundishwa ni: nukta, alama ya mshangao, kimilikishi, koma, alama za kunukuu.*

Sentensi zinazoweza kuonyeshwa kwa urahisi:


*Nukta – Mwanamume anaona nyoka.* 

*Alama ya mshangao – Mwanamume anaona nyoka!* 

*Umilikishi – Mwanamume anaona kalamu ya mwanamume.* 

*Mwanaume anaona kalamu ya mwanamke.* 

*Koma na alama za nukuu – Mwanadamu anasema, "Naona kalamu."*



Wakati wawezeshaji wakitumia kadi zao za Maandiko kwa somo hili, wasome pamoja Maandiko kutoka Marko 7:32-35.

Watu wamleta kiziwi bubu mwanaume (kwa) Yesu.
Watu wanamwomba Yesu aweke mkono juu ya mtu huyo.
Yesu alimleta mtu huyo mbali na umati.
Yesu aliweka mkono (wake) ndani ya masikio la mtu.
Yesu akatema mate.
Yesu aligusa ulimi wa mtu.
Yesu alitazama juu mbinguni.

Yesu akahema.
Yesu alisema, “Funguka!”
Masikio la mtu lilifunguliwa.
Ulimi wa mtu ulikuwa huru.
Mwanaume alizungumza vizuri.

<u>Kufundisha Alama Mpya Mchanganyiko</u>


- *Wakati wa kufundisha alama mpya mchanganyiko, ni muhimu kutambua alama zote za msingi zilizomo humo.*
- *Alama hii mchanganyiko inaweza kuwa na alama badilifu.*
- *Alama hii mchanganyiko inaweza kuwa na alama moja au zaidi mchanganyiko ndani yake.*

*Wanafunzi wanapoweza kuona vitu hivi katika alama mpya mchanganyiko, itawasaidia kuwa na ufahamu zaidi wa maana yake. Kadiri wanafunzi wanavyoelewa alama mpya mchanganyiko, ndivyo wanavyoweza kukumbuka kwa urahisi zaidi.*

*Tutafanyia kazi baadhi ya mifano. Hii itakuwa muhimu sana kujua jinsi ya kufanya wakati unapotayarisha masomo mapya! Katika kamusi alama mchanganyiko zina taarifa katika mabano ambazo zina manufaa.*


Andika alama zifuatazo kwenye ubao mweupe,<u> lakini usiwafunulie maana yake wawezeshaji hadi watakapofanyia kazi kutafuta alama za msingi na alama zozote badilifu na/au alama za ziada mchanganyiko.</u>


